Usiteleze kwenye Barabara ya UKIMWI



Usiteleze kwenye Barabara ya UKIMWI

Wazo la hadithi: Rakesh Rajani, Krista Riber, Veena Gokhale
Mwandishi: Veena Gokhale
Mfasiri: Martha Qorro
Mchoraji: Marco Tibasima
Wachangiaji: Robert Mihayo, Honaratus Swai, Godfrey Telli, Richard Lucas, Agnes Mangweha, Pius Makomelelo, Maria Kalavo, Mary Nsemwa, Kajubi Mukajanga
Mhariri: Rakesh Rajani

@ HakiElimu 2006
SLP 79401, Dar es Salaam, Tanzania
Barua pepe: info@hakielimu.org
Tovuti: www.hakielimu.org

ISBN 9987-423-33-7

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa minajili isiyo ya kibiashara. Unachotakiwa kufanya ni kunukuu chanzo cha sehemu iliyonakiliwa na kutuma nakala mbili kwa kila mchapishaji.

Dibaji

Kuzuia virusi vya Ukimwi na Ukimwi kwa ujumla ni changamoto kubwa. Je, ni njia zipi zitasaidia kuzuia Ukimwi? Ni kwa jinsi gani kila mmoja wetu ataonesha kumjali mwenzie? Kujua ukweli juu ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi wenyewe ni hatua ya kwanza tu ya kuudhibiti. Mawasiliano ya wazi kwa rika zote juu ya mapenzi, ngono, urafiki na ndoa ni muhimu kama jamii inataka kukabiliana na virusi vya Ukimwi na Ukimwi wenyewe.

Vijana wanahitaji mbinu na ujuzi wa kuwasaidia kushinda katika maisha. Wanapaswa kujiamini, kuwa na matumaini, kuwajibika na kuwa wabunifu. Zaidi ya yote, watu wanapaswa kujadiliana na kusikilizana.

Kitabu Usiteleze Kwenye Barabara ya Ukimwi kinatumia majadiliano ya abiria wananaosafiri kwa daladala kufikisha ujumbe huu. Kinaonesha kuwa wakati wote kutakuwa na mawazo ya kukinzana dhidi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi. Tunaweza kupingana na kutoafikiana. Lakini muafaka na mabadiliko vinawezekana.Pamoja na tofauti zetu hizi tunaweza kuwa wamoja na kuhudumiana.

Tunawahimiza wanafunzi, walimu, vijana na watu wote kukitumia kitabu hiki kujadiliana juu ya kipi kifanyike na mbinu zipi zitumike katika kukabiliana na tatizo hili. Kila mmoja wetu anaweza kuleta mabadiliko.

Tungependa sana kusikia kutoka kwako. Hivyo tafadhali jibu maswali yaliyopo mwishoni mwa kijitabu hiki kisha tuandikie maoni yako.


WAHUSIKA WA HADITHI HII





SHULE YA MSINGI
WATOTO



Pambana na UKIMWI
Jizuie hadi kufunga ndoa!



Pambana na UKIMWI
Jizuie hadi kufunga ndoa!
Tangazo gani! Ndoto za mchana; kana kwamba vijana watasubiri!
tai LIMITED
Sawa, wapo wenye maoni hayo... Lakini... Mimi sipendi sana pia...


Nakuambieni ninyi; ujumbe huu hautafanikiwa!
Nimeliona hili tangazo kwenye luninga pia. Shangazi yangu alilipenda. Alisema ni njia sahihi ya kupambana na UKIMWI.
DAWA


Huu ni upuuzi! Vijana wangapi mnaowafahamu wenye kujizuia ?
Najua baadhi, washika dini sana, au wenye wazazi wakali mno.
Na baadhi wenye haya, wengine huenda hawana rafiki wa kiume au wa kike...



Lakini je, vijana wengi watawezaa kupokea ujumbe wa namna hii? Je, si wakati muafaka sasa kutoa ujumbe utakaosaidia vijana kupambana na UKIMWI?
DUKA
Ndiyo! Nakubaliana nawe! Ningefurahi kufahamu ujumbe huo na kuwafahamisha wengine!


Twendeni na hii daladala, tukutane na kujadiliana na watu mbalimbali, na tuone kama tutapata jawabu!
?
!
Chip



Mwenge! Mwenge! Basi la Mwenge!
Sawa!



tai
Usijali.
Mambo safi!




Tunasemaa... nini hasa kitasaidia watu kupambana na UKIMWI?
Labda tuzungumzie UKIMWI kwa uhuru zaidi?


HE!
AAGH!
EHEE!
MH!
LEO?!



Nimefurahi unasema hivyo. Nadhani itasaidia kuzungumzia kujamiiana, upendo, kukua, vyote hivyo kwa uwazi zaidi.
Mnasemaje? Watoto kuzungumzia mambo hayo? Na watu wazima wakaitikia? Huo siyo utamaduni wetu!



Eti bibi, ni kweli kwamba takriban nusu ya wanafunzi wote wa shule za msingi nchini hufanya ngono?
Tunaambiwa kwamba watu wengi wanaokwenda hospitalini- hata watoto wadogo- wameathirika kwa UKIMWI, ni kweli?
Ni wale tu wanaofanya mambo mabaya ndio wanaopata UKIMWI!


Unategemea nini kwa vijana?
Je, kuwa na rafiki wa kiume
ni vibaya?


Vijana wana wajibu pia. Na watu wazima ni lazima tuwasaidie kujifunza kuwajibika. Ndiyo maana uwazi ni muhimu.
Kama vijana wangepata fursa ya kujadiliana juu ya nyendo zao kuhusu UKIMWI, hali ingebadilika. Ni kweli bibi?
HII NI OFISI KAMA OFISI NYINGINE. SHESHIMU!


Simama! Simama!




Habari! Mnakwenda wapi?
Tunatafuta majawabu ya tatizo la UKIMWI!


Kwa hiyo ninyi wawili mnafikiri nini kitasaidia?
Nafikiri jawabu liko pale katika bango la matangazo.
Bright Future
COMPUTER COLLEGE
Diploma ya Bright Futu
Itakuhakikishia kazi nzuri kwa


Una maana gani? Kwa vipi kozi ya kompyuta inasaidia kupambana na UKIMWI?
Itakupa ujuzi na ajira, utajisikia vizuri.


Lakini hiyo ni kwa matajiri! Je, kwa kijana maskini kama mimi?
Bado unaweza kufanya mambo. Sikufanikiwa kwenda sekondari na wala sina ajira lakini simwogopi yeyote!


Anachosema ni sawa! Siyo lazima kujifunza kompyuta. Unaweza kujifunza ujuzi mwingine... kwa msaada wa familia au hata serikali...


Nimekuwa nikijihusisha na biashara ndogo ya kufuga na kuuza kuku. Biashara hii imeniwezesha kulea wanangu watano. Siku zote najitahidi kuwa muwazi kwao.


Mara basi linasimama...
Usiteleze ukaangukia kwenye
Barabara ya UKIMWI


Mnajua jawabu langu?
Kupiga au kutengeneza
muziki poa!





Mnasema nini? Ni muziki huu huu na dansi, kusherehekea na kunywa usiku kucha ndivyo vinavyosababisha UKIMWI!
Hapana, havisababishi!!
TIBASIMA ARTS INV. LTD



Ndivyo vinasababisha, nimefahamu vijana wa namna hiyo huishia pabaya kweli... nitahakikisha kuwa mwanangu hafuati mwenendo huo.


Lakini ninafahamu vijana ambao wangekuwa wameharibikiwa saa hizi, kama siyo kwa kugundua njia ya kuwa wabunifu kuyaeleza matatizo yao!



Muwe wabunifu, lakini muwe wenye kuwajibika. Fikiri! Usifuate tu mkumbo wa wenzako bila kufikiri.
Lakini, watu wazima wote huwa siku zote wana-fanya mambo sahihi?


Sawa. Siyo watu wazima wote wanatenda kama watu wazima! Wanahitaji kubadilika pia.
HESHIMU KAZI
KANDA


BREKI!
Hebu tutoke wote! Napenda niwaambie jambo.
Natumaini siyo pancha. Nitachelewa!


Niliyaandika maandishi haya mwaka mmoja uliopita wakati nilipogundua kwamba nimeathirika na UKIMWI.
!
!
!
?
!
!
Usiteleze ukaanguka kwenye
Barabara ya UKIM


Nimefurahi kuwa mmesafiri kwa daladala langu na kutoa majawabu haya. Nafikiri tuyaandike kwenye basi kila mmoja aweze kuyaona.
Sawa!
Mr. Thomas
Box 10
Tz.



- Kutia moyo = maisha
- Kuwa wa kujieleza na mwenye kuwajibika, jifikirie
- Kuwa mwenye nguvu
- Jifunze ujuzi, jiamini, chuma pesa pia!
- Kuwa mbunifu na msanii – thubutu kufikiri
- Subiri kama utaweza lakini usifanye kamwe bila kondomu!
- Watu wazima; zungumza kwa matendo mema siyo maneno matupu
- Zungumza na marafiki, majirani, walimu, wazazi, ndugu; uwazi = afya


Usiteleze na kuanguka kwenye barabara ya UKIMWI. Mtunzane mpaka mwisho kabisa!

Leta Mawazo!
Usiteleze kwenye Barabara ya UKIMWI

Tarehe iliyopokelewa……...…….

Jina…….....……

Anwani ya Posta……....……

Namba ya simu…….....…….

Barua pepe…….....…….

Jinsi ☐ Mme ☐ Mke

Umri
- ☐ 7 – 14
- ☐ 15 – 19
- ☐ 20 – 30
- ☐ 31 – 40
- ☐ Zaidi ya 41

Kiwango cha Elimu
- ☐ Elimu ya Msingi
- ☐ Elimu ya Sekondari
- ☐ Chuo

1. Kitabu hiki kina habari muhimu?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
2. Kitabu hiki kina manufaa?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
3. Kitabu hiki kinaeleweka kiurahisi?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
4. Kitabu hiki kinavutia?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
5. Kitabu hiki kimeandikwa vizuri?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi
6. Umependa michoro ya kitabu hiki?	☐ Ndio	☐ Hapana	☐ Kiasi

Umependa nini kwenye kitabu hiki?

Kitabu hiki kinawezaje kuboreshwa?

Unategemea kutumiaje kitabu hiki?

Mengineyo:

Ukimaliza kujaza formu hii itume: HakiElimu, Uchapishaji, SLP 79401, Dar es Salaam

Usiteleze Kwenye Barabara Ya Ukimwi ni hadithi juu ya njia tunazoweza kutumia kujikinga na Ukimwi. Ni majadiliano kati ya marafiki na wasafiri- vijana na watu wazima ndani ya daladala. Watu wana mitazamo tofauti juu ya suala hili. Wanabishana na wakati mwingine wanashindwa kuafikiana kipi kinafaa na kipi hakifai. Ghafla dereva wa daladala anasimamisha gari na kuonesha jambo fulani….Soma ujue nini kitaendelea.



HakiElimu inafanyakazi kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu na jamii. Tunafanya hivyo kwa kuwezesha jamii kupata habari kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera; kuchochea ubunifu wa mijadala ya umma; kufanya utafiti yakinifu uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kuendeleza manufaa ya pamoja na kuzingatia haki za jamii.

Barabara ya Mathuradas 739 • Upanga
SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org
Simu: (255 22) 2151852 au 3 • Faksi: 2152449